Taarifa kwa vyombo vya habari | 19 February 2024

Mpango wa Motisha kwa Walimu unaotekelezwa na Twaweza umesaidia zaidi ya wanafunzi 77,000 katika kuboresha umahiri wao kwenye stadi za Kusoma na Kuhesabu.

Walimu pamoja na walimu wakuu wamelipwa jumla ya shilingi milioni 401 kama motisha ya ufundishaji juu ya mishahara yao.

Wiki hii, walimu katika shule za msingi 265 kwenye mikoa 11 ya Tanzania wamepokea jumla ya shilingi milioni 401 kwenye akaunti zao za benki ikiwa ni motisha kulingana na utendaji wao. Kiwango cha motisha wanayolipwa walimu kinategemea umahiri uliooneshwa na wanafunzi wao katika majaribio ya kusoma na kuhesabu yaliyofanyika mwishoni mwa mwaka wa masomo - 2023.

Takribani walimu 1,044 wamelipwa jumla ya shilingi milioni 334.4. Kwa wastani, mwalimu wa masomo hupokea TZS 320,000 (USD 128), ambayo ni sawa na 3.4% ya wastani wa mshahara wa mwaka wa mwalimu. Kiasi kinachopokelewa na kila mwalimu kinategemea idadi ya wanafunzi wanaomudu stadi za msingi katika darasa lake ikiwa ni pamoja na kusoma hadithi, kujumlisha, na kutoa, kama inavyotakiwa katika mtaala wa taifa.

Jumla ya walimu wakuu 273 wamepokea jumla ya shilingi milioni 67. Katika kutambua nafasi yao kiutendaji, walimu wakuu wanapokea bakshishi sawa na asilimia 20 ya kiwango wanacholipwa walimu wa masomo katika shule zao.

Motisha hii ya utendaji wa walimu inalipwa kupitia programu inayoitwa KiuFunza (Kiu ya Kujifunza), inayotekelezwa kwa ushirikiano kati ya shirika la Twaweza na Serikali ya Tanzania, wakiungwa mkono na taasisi ya Hempel ya Denmark. Programu ya KiuFunza inalenga kuboresha ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuhesabu kwa wanafunzi wa madarasa ya 1, 2 na 3. Dhima ya mpango huu ni kuwawezesha watoto wote nchini Tanzania kumudu stadi za kusoma na kuhesabu wafikiapo umri wa miaka 10.

Shule 265 zilizopo kwenye mpango huu kwa sasa zilichaguliwa kwa njia ya nasibu kutoka katika wilaya zenye matokeo ya chini zaidi katika mikoa na halmashauri za Tanzania, kwa mujibu wa takwimu rasmi za tathmini ya Taifa ya darasa la nne.

Viwango vya ufaulu katika shule zilizopo kwenye mpango wa KiuFunza tayari vimeanza kuimarika. Mnamo mwezi Novemba mwaka 2023, kabla ya mzunguko wa kwanza wa malipo ya motisha, wanafunzi katika shule za mpango walionesha umahiri zaidi kwenye stadi za kusoma na kuhesabu, ikilinganishwa na shule zilizo kwenye kundi linganishi (control) ambazo pia zilianza mwaka wa masomo katika kiwango kile kile cha umahiri.

Matokeo ya ujifunzaji kwa mwaka 2023 yamekuwa ya kiwango cha juu cha ufaulu kwenye madarasa yote matatu katika shule za mpango ikilinganishwa na shule linganishi. Katika somo la KUSOMA, viwango vya ufaulu ni 44% katika kundi linganishi na 49% katika shule za mpango. Hivyo basi, kuna ongezeko la +5% kwenye ujifunzaji wa stadi za kusoma. Katika somo la HESABU, viwango vya ufaulu ni 45% katika shule linganishi na 52% katika shule za mpango wa KiuFunza; ongezeko la ujifunzaji kwa mwaka 2023 ni +7%.

Katika awamu iliyopita ya mpango huu, mfumo sawa wa utoaji motisha ulitumika lakini ilikuwa katika shule 100 pekee. Matokeo ya mzunguko wa kwanza wa utekelezaji wa KiuFunza 4 (2023) ni sawa na yale yaliyopatikana mwaka 2019, katika mzunguko wa kwanza wa utekelezaji wa awamu ya 3 ya mpango wa KiuFunza, hata hivyo, awamu ya sasa inashirikisha zaidi ya mara tatu ya idadi ya shule.

Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza, alisema *"Kujifunza ni jambo muhimu kwa maendeleo yetu ya kitaifa: watoto wetu wote wanapaswa kumudu stadi za kusoma na kuhesabu wafikiapo umri wa miaka 10. Bila shaka, tunahitaji shule nzuri, ufundishaji mzuri na vitabu, lakini mara nyingi watu husahau kwamba tunahitaji walimu waliohamasika pia, ili kufikia malengo. Tumedhihirisha kwenye utekelezaji wa KiuFunza kwamba tunaweza kupanua mfumo rahisi wa motisha kwa walimu kutoka shule 100 hadi karibu shule 300 kote Tanzania na bado tukapata matokeo makubwa ya ujifunzaji, hii ikiifanya KiuFunza kuwa moja ya mipango yenye gharama nafuu zaidi katika kuimarisha na kukuza stadi za msingi."*

"KiuFunza pia inashughulika na changamoto za usawa katika mifumo: walimu wa Darasa la 1, 2 na 3 wana jukumu la kuweka msingi wa kusoma na hesabu kwa watoto wetu. Lakini wana madarasa yenye idadi kubwa sana ya wanafunzi. Walimu wa madarasa ya awali wanapata takribani 40% pungufu ya mishahara ikilinganishwa na wenzao wa shule za msingi katika madarasa ya juu (IV-VII). Tunatatua changamoto hii ya usawa kwenye malipo si kwa kuongeza mishahara yao ya msingi bali kupitia malipo ya motisha kwa kadri ya utendaji wao. Kutokana na kwamba inalipwa kwa kuzingatia umahiri wa mwanafunzi mmojammoja, darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi linageuka kuwa kivutio kwa walimu."

--Mwisho—

Kwa mawasiliano zaidi: Annastazia Rugaba | Barua pepe: arugaba@twaweza.org | simu: (+255) (0) 687 222 197

Dokezo kwa Wahariri

- Twaweza inafanya kazi kuwawezesha watoto kujifunza, wananchi kusikilizwa na serikali kuwa wazi zaidi na sikivu nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Tuna program mbalimbali, wafanyakazi na ofisi katika nchi zote tatu, na utaratibu unaoheshimika duniani wa kujifunza, ufuatiliaji na tathmini. Programu zetu ni pamoja na KiuFunza, mojawapo ya majaribio makubwa na yenye matumaini zaidi barani Afrika ya kuboresha ujuzi wa msingi wa kusoma na kuhesabu katika shule za msingi za umma, na Sauti za Wananchi, utafiti wa kwanza wa simu za mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa barani Afrika. Tunatekeleza ushiriki wa umma na sera kwa ufanisi, kupitia ushirikiano wenye nguvu pamoja na vyombo vya habari na uongozi wa kimataifa wa mipango kama Ushirikiano wa Serikali Wazi (OGP), Ushirikiano wa Kimataifa kwa Data Endelevu ya Maendeleo (GPSDD), na Ushirikiano wa Ufichuzi wa Mikataba (OCP).

- Unaweza kufuatilia kazi ya Twaweza kupitia:
  Tovuti: www.twaweza.org Facebook: Twaweza Tanzania Twitter: @Twaweza_NiSisi